WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO CHA UALIMU BUTIMBA

Tovuti: www.butimbatc.ac.tz

Baruapepe: butimbatc@moe.go.tz

Mkuu wa Chuo,

Chuo cha Ualimu Butimba,

S.L.P. 1411,

MWANZA

Unapojibu tafadhali rejea;

Kumb.Na.BCE/ET/37/94/89

29 APRILI, 2021

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA MAALUM YA UALIMU SEKONDARI NA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA SEKONDARI JULAI / AGASTI 2021

1.0: UTANGULIZI: -

Napenda kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya STASHAHADA MAALUM YA UALIMU SEKONDARI / STASHAHADA YA UALIMU ElIMU YA SEKONDARI katika chuo cha Ualimu Butimba. Chuo kinakupongeza kwa nafasi hii. Tunategemea kuwa utatumia nafasi hii vizuri wakati wote wa mafunzo yako. Hivyo, unaelekezwa kuweka jitihada na kutumia maarifa na rasilimali zilizopo kufanikisha ndoto zako binafsi na zile za Taifa kwa ujumla.

2.0: MAHALI CHUO KILIPO: -

Chuo kipo mkoa wa Mwanza katika Halmashauri ya jiji la Mwanza kilometa nane (08) kutoka mjini kati. Kuna njia kuu tatu zitakazokuwezesha kufika chuoni. Iwapo unatokea mjini kati panda basi za umma (daladala) zilizoandikwa BUTIMBA TTC ambazo zitakufikisha hadi lango kuu la kuingia chuoni. Iwapo unatokea stendi kuu ya mabasi Nyegezi panda daladala zinazoelekea mjini, shuka kituo cha Mkuyuni sokoni (Butimba Kona) au iwapo utatokea stendi ya kuu ya mabasi Buzuruga pia shuka Mkuyuni Sokoni (Butimba Kona) na hapo utapata usafiri mwingine wa daladala zitokazo mjini Mwanza kwenda chuoni Butimba. Pia upo usafiri wa taxi kutoka hapo Butimba kona. Tusingeshauri sana usafiri wa bodaboda ambao pia unapatikana.

3.0: TAREHE YA KURIPOTI: -

Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga mafunzo ya Stashahada Maalum ya Ualimu Sekondari wanatakiwa kuripoti Chuoni tarehe 15/07/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 29/07/2021. Baada ya tarehe hiyo, mwanafunzi aliyechelewa atapoteza sifa za kujiunga na Chuo.

Aidha, wanafunzi waliochaguliwa kujiunga mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Sekondari wanatakiwa kufika chuoni tarehe 15/08/2021 na mwisho wa kuwapokea itakuwa tarehe 29/08/2021. Baada ya tarehe hiyo, mwanafunzi aliyechelewa atapoteza sifa za kujiunga na Chuo.

3.1: USAIILI: -

Mwanachuo afikapo Chuoni, lazima aripoti kwa Msajili wa wanachuo kwa ajili ya kusajiliwa. Mwanachuo anayeripoti chuoni haruhusiwi kwenda Bwenini au maeneo mengine ya chuo kabla ya kupewa utaratibu kutoka Ofisi ya Usajili.

4.0: MUDA WA MAFUNZO: -

4.1 Wanachuo waliochaguliwa kujiunga na Stashahada ya Maalum ya Ualimu Sekondari kwa sifa za kidato cha nne, watakuwa mafunzoni kwa muda wa miaka mitatu (2021 - 2024).

4.2 Wanachuo waliochaguliwa kujiunga mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Sekondari (Sayansi na Sanaa) kwa sifa za kidato cha sita, watakuwa mafunzoni kwa kwa muda wa miaka miwili (2021 - 2023).

4.3 Wanachuo waliochaguliwa kujiunga mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Sekondari (Fani) kwa sifa za kidato cha sita, watakuwa mafunzoni kwa muda wa miaka miwili (2021 - 2023).

NB. *Fani (somo mojawapo lenye ufaulu wa juu miongoni mwa yale uliyofanyia mtihani kidato cha sita pamoja na chaguo lako moja katika sanaa za ufundi (Fine arts), muziki (Music education), sanaa za maonesho (Theatre arts) au elimu kwa michezo (Physical education).*

5.0: MAHITAJI BINAFSI YA MWANACHUO: -

- Shuka jozi 2 za rangi ya buluu na mto wenye foronya ya buluu.
- Ndoo.
- Chandarua cha mbu.
- Daftari 8 (Counterbook quire two)
- Bukta ya buluu, fulana nyeupe na tracksuit ya buluu.
- Raba nyeupe za michezo.
- Sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
- Hati ya uthibitisho wa Daktari (imeambatanishwa).
- Scientific calculator kwa wanafuzi wa masomo ya sayansi
- Vifaa vya michezo, ala za muziki au maleba (mojawapo ya hivi kwa waliochaguliwa mafunzo ya Fani).
- Koti jeupe la maabara (wanachuo wanaosoma Sayansi).

6.0: VYETI:

- Mwanachuo afike chuoni na **CHETI HALISI (Original Academic Certificate)** cha Kidato cha NNE kwa wahitimu wa kidato cha nne au cheti cha kidato cha NNE na SITA kwa wahitimu wa kidato cha sita.
- Mwanachuo aje pia na ***'Leaving Ce rti fi ca te'*** yake ya shule aliyomaliza kidato cha Nne na cha Sita isipokuwa kama alikua mtahiniwa wa kujitegemea (private candidate). MWANACHUO ASIPOKUJA NA VYETI TAJWA HAPO JUU, HUTAPOKELEWA CHUONI.

ANGALIZO: Ikiwa mwanachuo ni Mtumishi (mwajiriwa) aje na kitambulisho chake halisi cha kazi na barua ya ruhusa kutoka kwa mwajiri wake.

7.0: ADA YA CHUO:

Ada ya Chuo ni Tshs. **450,000/=** kwa mwaka. Ada hii inaweza kulipwa kwa awamu mbili yaani Tshs. **225, 000/=** kwa muhula au unaweza kulipa kiasi chote Tshs. **450,000/=** mara moja kwa mwaka.

Ada ya Chuo ilipwe kwa namba ya kumbukumbu (control number) inayotolewa na ofisi ya uhasibu. Mawasiliano na ofisi ya uhasibu kupata namba ya kumbukumbu yafanyike kwa namba: **0786 441 736**.

8.0: MICHANGO MINGINE Y A CHUO:

Na.	**MCHANGO**	**KIASI (TSH)**	**MAONI**
i	Serikali ya wanachuo	5,000.00	Mwaka
ii	Huduma ya kwanza	10,000.00	Mwaka
iii	Usafi na mazingira	20,000.00	Mwaka
iv	Kukodi godoro	10,000.00	Mwaka
v	Usajili na kitambulisho	20,000.00	Mwaka wa kwanza tu
vi	Michezo	30,000.00	Mwaka
vii	Ulinzi	30,000.00	Mwaka
viii	Ukarabati	25,000.00	Mwaka
JUMLA		**150,000.00**	

Fedha yote ya michango iliyoorodheshwa (kipengele 8.0) hapo juu ilipwe kwenye akaunti ya michango ya Chuo **Na: 31101200023 Benki ya NMB.** Jina la akaunti ni ***Butimba Teachers Training College.***

MUHIMU SANA:
Baada ya kufanya malipo ya ada na michango, mwanachuo awasilishe ofisi ya usajili ***'Bank*** **Pay in Slip' au** Stakabadhi inayotolewa na Benki husika, moja ikiwa ni ya

malipo ya ada ya chuo na nyingine ni ya malipo ya michango mingine ya chuo. Ukichanganya malipo hayo hutarudishiwa fedha yako na itakubidi ulipe mara mbili (fanya malipo sahihi kwenye akaunti husika). Vilevile, stakabadhi za malipo zionyeshe jina kamili la mwanachuo husika.

Inashauriwa uwe na kadi ya bima ya Afya kwa ajili ya uhakika wa huduma ya matibabu kutoka katika hospitali yoyote na mahali popote utakapokuwa.

9.0: VIFAA VINGINE KWA AJILI YA MATUMIZI YA CHUO:

Kila mmoja aje na v i f a a v i f u a t a v y o:

i. Bunda (01) la karatasi (**Double A/Mondi Rotatrim/Smart Copy**).
ii. Flat file (01)

10.0: SARE YA CHUO

A. Wanawake:

- Sketi nyeusi mbili (0 2) zenye kuvuka magoti sm 3 zikiwa na rinda moja tu (Tazama mchoro Na. 1 hapo chini).
- Shati mbili (0 2) zenye rangi ya buluu bahari (light blue) mikono mirefu.
- Koti la suti rangi nyeusi.
- Tai ndefu nyeusi mbili (0 2).
- Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi jozi mbili (02).
- Soksi nyeupe jozi mbilii (02).

Angalizo: Kwa wanachuo wanaovaa hijab, suruali mbili nyeusi pana, blauzi ndefu kuvuka magoti na kitambaa cha kichwani rangi ya buluu bahari (light blue). Kanga na mitandio siyo sehemu ya hijab kwa mujibu was sare za chuo .

B. Wanaume:

- Suruali nyeusi mbili (02) zenye marinda (Tazama mchoro Na.2 hapo chini).
- Shati mikono mirefu m b i l i (0 2) rangi ya bluu bahari
- Tai nyeusi mbili (02) .
- Viatu vyeusi jozi mbili (0 2).
- Soksi nyeusi jozi m b i l i (02) .
- Koti la suiti rangi nyeusi.

Mchoro Na. 1



Mchoro Na. 2



NB: T-shirts yenye nembo ya chuo itapatikana chuoni kwa kiasi cha shilingi **15,000.00** tu. Fedha hii ilipwe kwenye akaunti ya michango **Na: 31101200023 Benki ya NMB.** Jina la akaunti ni ***Butimba Teachers Training College.***

11.0: USAFIRI:-

Nauli ya kuja chuoni na kurudi nyumbani itagharimiwa na mwanafunzi husika.

12.0: CHAKULA:-

12.1: Chuo kinatoa huduma ya chakula kufuatana na uwezo wa serikali.

12.2: Chuo hakiruhusu wanachuo kujipikia mabwenini au mahali popote katika eneo la chuo. Hivyo USIJE NA SUFURIA AU JIKO LA KUPIKIA.

12.3: Chuo hakina chakula maalum **(special diet)** kwa wanachuo wenye changamoto za kiafya.

13.0: MAWASILIANO:

Mawasiliano yoyote yanayomuhusu mwanachuo kutoka kwa ndugu, jamaa na marafiki **LAZIMA** yapitie kwenye uongozi wa Chuo, kwa Namba: **0767-211902** (Msajili wa Wanachuo), **0787-412589** (Msajili Msaidizi), **0784251553** (Mwadili wa Wanachuo) na **0784-630187** (Mwadili Msaidizi)

14.0: **NIDHAMU**

Wakati wote uwapo hapa Chuoni unatakiwa kufanya mambo sahihi kwa wakati sahihi, kuwa mahali sahihi, na kupita njia sahihi kwa mujibu wa **KANUNI/TARATIBU** za chuo ambazo utazipata mara ufikapo Chuoni.

11: **MWISHO: -**

Tunategemea kuwa utakuwa mfano mzuri wa kuigwa na wanachuo wenzako, walezi na jamii kwa kutekeleza **"MOTTO"** wa Chuo **"]UHUDI NA MAARIFA".**

KARIBU CHUO CHA UALIMU BUTIMBA

NICHOLAS A MAGIGE

MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU BUTIMBA
S. L. P. 1411 MWANZA

Nakala: Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo cha Ualimu Butimba

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY
BUTIMBA TEACHERS COLLEGE

Website: www.butimbatc.ac.tz
Email:butimbatc@moe.go.tz

Principal,
Butimba Teachers College,
P.O.Box 1411,
MWANZA

In reply please refer:
Ref.No.BCE/ET/37/94/89

29th APRIL, 2021

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

To the Medical Officer; ……..

Please examine *Mr/Mrs/Miss …… (Name in Full) as to his/her physical and mental fitness for enrolment as a student teacher.

The examination should include but not limited to the following categories:

1. (a) Eye sight (b) Hearing
   (c) Speech (d) Venereal Diseases
   (e) Leprosy (f) Limbs
   (g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Blood Group
4. Pregnancy (if applicable)
5. Other medical condition (s)

PARTB: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by Government Medical Officer)

1. (a) Eye sight ……..
   (b) Hearing ……..
   (c) Speech ……. …
   (d) Venereal Diseases ……
   (e) Leprosy ……..
   (f) Limbs ……..
   (g) Epilepsy ……..
2. Neuroses……
4. Blood Group ……
5. Pregnancy (if applicable) ……..
6. Other medical condition (s)……..

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally*fit/unfit for enrolment as a student teacher.

Date: …… Station……..……..……

Designation …… Signature and Stamp ……..……